

A WIVU WA MATESO YAKE.

- ❖ Wayahudi hawakuweza kupinga ujumbe wa Stefano juu Masihi Yesu, hivyo wao hususani Paulo wakakerwa.
- ❖ Hawakuweza kumkabili Stefano na ukweli, hivyo wakapata mashahidi bandia waliomtuhumu kwa kuiongelea vibaya Sheria na Hekalu (Matendo 6:11-14).
- ❖ Sauli kijana, alikubaliana na hukumu ya Baraza. Alishuhudia kupigwa mawe kwa Stefano na kukubali (Matendo 7:58; 8:1).

B UONGOFU WAKE.

- ❖ Sauli alilitesa kanisa kwa hasira yenye ukatili-aliyodhani ni wivu wa dini.
- ❖ Akili yake ilidumu katika kuharibu mafundisho potofu, lakini dhamira yake ilimwambia kuwa Stefano hakuwa na hatia na fikra yake ilikuwa sahihi.
- ❖ Kila kitu kilibadilika njiani akielekea Dameski. Yesu alitokea kwake na kumuonyesha neema Yake. Udhuru wote kichwani mwake wakumkataa Masihi aliyesulubiwa ulitoweshwa.

C UZOEFU WAKE DAMESKI.

- ❖ Sauli alikaa nyumbani mwa Yuda siku tatu akiwa kipofu. Kama Anania alivyosema, Wakristo walidhani kuwa alikuwa akijifanya kipofu ili awanase ghafla.
- ❖ Yesu alimwonesha Anania kuwa Sauli alikuwa dhati kabisa. Baada ya kupata kuona tena, Anania alimwalika kuyakabidhi maisha yake kwa Yesu na kuonyesha hilo kwa njia ya ubatizo. (Matendo 22:16)
- ❖ Sauli alitaka kusitisha Imani ya Kikristo Dameski, lakini aliongolewa kuwa mtetezi wa Kristo, na kueneza Injili duniani kote.

D UTUME WAKE KWA MATAIFA.

- ❖ Kampeni ya kwanza ya kimishonari miongoni mwa Wamataifa ilianza hapo; ilizaa matunda mengi sana.
- ❖ Wakristo wa Yerusalemu waliposikia juu ya mafanikio hayo, walimtuma Barnaba hapo. Aliona fursa katika mji huo na kumuita Sauli aje kumsaidia.
- ❖ Kanisa liliposimikwa na kukawa na viongozi wakutosha wakuliegemeza, Roho Mtakatifu alimwita Sauli kuhubiri Injili kwa watu wa Mataifa.

E MGOGORO WAKE NA KANISA.

- ❖ Kidogo kidogo Injili ilihubiriwa kote katika ulimwengu uliyofahamika.
- ❖ Lakini kukaibuka swali: Tufanya nini na Wamataifa? Je, watahiriwe na kutunza sheria ya Musa? Je, inatosha tu, kuwa na Imani katika Yesu?
- ❖ Baraza la Yerusalemu(Matendo 15) lilijitahidi kuweka bayana maswali haya. Hata hivyo, Mafarisayo wakaidi waliendelea kuhubiri mawazo yao.
- ❖ Na huo ukawa msingi wa waraka kwa Wagalatia.